



MACHAKOS UNIVERSITY

University Examinations for 2019/2020 Academic Year

SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES

DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES

DECEMBER SESSION EXAMINATION FOR

BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

AKS 0104: INTRODUCTION TO KISWAHILI LITERATURE

TAREHE: 16/11/2020

MUDA: 8:30 – 10:30 AM

***Maagizo:* Jibu swali la kwanza na mengine mawili**

- | | | |
|----|---|------------|
| 1. | a) Elezea chimbuko la sanaa kwa kuzingatia mtazamo wa kidhaniifu
na mtazamo wa kiyakinifu. | (alama 10) |
| | b) Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yafuatayo. | (alama 20) |

Nimeona, milima na mabonde,misitu na nyika,
Nimeona, majani na umande,uliotandazika,
Nimeona, mkulima yuwenda shambani.

Nimeona, uwanda na magugu, yalomkabili,
Nimeona,wajibu na vurugu,’wiano mkali
Nimeona, mkulima akiwa tayari.

Nimeona, kwa ari na juhud, anatupa jembe,
Nimeona, kakaza ukaidi, kwa nguvu achimbe,
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Nimeona, kijua kinawaka, kama jahanamu,
Nimeona, jembe lainuka, linapohujumu,
Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminika, naye hatohis,
Nimeona, kwa kani anatimka, bila wasiwasi,
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao,
Na sioni, hadhiye kutukuka, ila kilio,
Kwa nini? Nauliza mkulima kwani?

MASWALI

- i) Shairi hili ni la bahari gani (alama 2)
 - ii) Fafanua maudhui yanayojitokeza katika shairi hili (alama 3)
 - iii) Eleza uhuru wa msanii katika shairi hili (alama 4)
 - iv) Eleza umbo la shairi hili. (alama 5)
 - v) Eleza mpangilio vina na mizani katika ubeti wa pili na wa tatu (alama 6)
2. a) Eleza dhima ya ngano katika jamii. (alama 10)
- b) Eleza istilahi zifuatazo za Fasihi .
- i) Kibwagizo
 - ii) Kikai
 - iii) Mandhuma
 - iv) Mhusika bapa
 - v) Mhusika hasidi
3. a) Fafanua aina kumi za tamathali za usemi katika kazi ya Fasihi. (alama 10)
- b) Eleza tofauti zilizopo kati ya Fasihi andishi na Fasihi simulizi. (alama 10)
4. Eleza tofauti zilizopo kati ya hadithi fupi na Riwaya ya Kiswahili. (alama 20)
5. a) Tambua vipera vya nyimbo katika jamii yako huku ukitoa mifano mwafaka. (alama 10)
- b) Huku ukitoa mifano , eleza aina tano za Tamthilia . (alama 10)